# *Yale Maandiko Ya Mkono Kwenye Ukuta*

Hakika ni vizuri kuwa ndani, asubuhi ya leo, katika sabato hii. Ni siku mbaya, lakini, hata hivyo, daima ni sabato kwa nafsi zetu tunapowazia juu ya Bwana na juu ya wema Wake.

2 Na sasa nimesema, leo, ya kwamba Bwana akipenda, ningependa kuhubiri Ujumbe wa asubuhi ya leo, kama ndugu yetu. . .hisani ya kuniruhusu nichukue i—ibada asubuhi ya leo, nasi tutazungumza asubuhi ya leo juu ya *Yale Maandiko Ya Mkono Kwenye Ukuta.*

3 Na, usiku wa leo, Bwana akipenda, nataka kuzungumza juu ya somo, *Je, Kanisa Litaenda Kabla ya Kipindi Cha Dhiki Kuu?* Na ningependa, ikiwa huna mahali popote ambapo—ambapo ungeenda kanisani leo, ama usiku wa leo, kwamba ungetokea usiku wa leo kwa ajili ya ujumbe, *Je, Kanisa Litakwenda Kabla Ya Kipindi Cha Dhiki?* Na mimi. . .Kuna mjadala mkubwa juu ya hilo, kama ndivyo au la kwamba Ka—Kanisa litaenda wakati huo, kwa hivyo tunataka kujadili hilo usiku wa leo.

4 Na sasa nilitoa, kwenye redio, jana, Ndugu yetu mpendwa Neville alifanya, kwamba asubuhi ya leo, kama kulikuwa na yeyote wa kuombewa, awepo hapa saa mbili. Naye mwanangu alikuwa tayari kutoa kadi, wala hapakuwa na mtu, hata mmoja. Saa tatu, kulikuwa na mtu mmoja tu wa kuombewa.

5 Sasa, usiku wa leo, iba-. . .ama kadi, kadi za maombi, zitatolewa. Nimefurahi kusikia hivyo. Nina furaha kuona wanajitayarisha kwa ajili ya mgonjwa mmoja, ambaye nitamwombea. Lakini kulikuwa na. . .Ibada usiku wa leo. . . Naam, labda ilikuwa asubuhi mbaya, na watu hawakutoka. Kwa hiyo, usiku wa leo, watakuwa wakitoa kadi za maombi saa kumi na mbili na nusu usiku wa leo, kwa hao. Kama. . . Tu—tunaweza kujua kwa hilo, basi, jinsi ya kuwekea msingi ujumbe wangu, kama utakuwa wa uponyaji wa Kiungu ama nini, juu ya. . .ama kubadilisha somo langu kuwa namna ya uponyaji wa Kiungu, ama iwe ni kwa ajili ya wokovu wa nafsi za watu tu.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, katika maombi.

6 Ee Mungu, Baba mwenye haki zaidi, tuna furaha sana asubuhi ya leo, tunapoingia katika patakatifu Pako, kutazama juu angani, kuona jinsi Wewe ulivyo mkuu, kama vile ndugu alivyoimba dakika chache tu zilizopita. Na kukuona ukitandaza mbawa Zako kubwa kutoka anga hadi anga, kama mama

tai alivyowatoa watoto wake kutoka kwenye kiota. Na kabla hajawachukua kutoka kwenye kiota, yeye hupeperusha tu mbawa zake kubwa nje, na kuacha watoto waone jinsi yeye alivyo mkuu, na jinsi alivyo na nguvu. Ndipo wanaweza kuamini mbawa zake, kwa sababu wanaruka kwa mara yao ya kwanza kutoka kwenye kiota chao.

7 Bwana Mungu, leo hii, tuna furaha sana kwamba tunaweza kutazama juu na kuona nyota angani, na—na mwezi, na mfumo mkuu wa jua unapozunguka katika upatanifu mkamilifu hivyo, ndipo tunaona jinsi Wewe ulivyo mkuu. Na inakuwa wakati wa sisi kuondoka kwenye kiota hiki cha ulimwengu, tuna ujasiri kujua ya kwamba Yeye aliyeziweka nyota katika njia zake, aliyeziumba mbingu na nchi, kwa hakika anaweza kuiongoza nafsi yetu isiyojiweza hadi mahali ambapo Yeye ameahidi, kwa kuwa tunaweza kuona jinsi Wewe ulivyo mkuu.

8 Na tunapojisikia ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, kabla tu ya Kuja kwa huyo Mwana Wako wa ajabu sana, huyo Mwokozi mpendwa, tunaomba, leo, ya kwamba utatukumbusha jinsi hili lilivyo karibu, tukio hili kuu. Na jalia kila nafsi humu ndani itupilie mbali tu kila wazo lingine wakati huu. Pia, Baba, tunaomba ya kwamba utasema nasi kupitia Neno Lako, leo, ili tupate kuona, kwa hekima ya manabii katika siku zilizopita, jinsi Kuja kwa Bwana kulivyo karibu sana.

9 Tunaposoma magazeti yetu, na kusikiliza redio, tunajua kwamba kuna kasoro. Na roho zetu zinatuambia kwamba kuna kitu kasoro kabisa.

10 Na utupe leo tunayohitaji. Waokoe wale, Bwana, wanaoweza kuokolewa leo. Na uwaponye wale wanaohitaji uponyaji leo. Nasi tunaomba ya kwamba utafungua masikio yetu kusikia Neno Lako. Fungua kinywa cha mtumishi Wako na useme sasa mambo ambayo yangetengwa kwa ajili ya Kanisa Lako katika saa hii. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu. Amina.

11 Huko katika Agano la Kale, katika Kitabu cha Danieli, mlango wa 5 na aya ya 25, ningependa kusoma. Na ninyi mnaoandika Maandiko yenu. Na sasa tunasikitika kwamba hatuna nafasi ya kutosha ya kuketi kwa wale waliosimama. Ninataka kusoma kutoka kifungu cha 25. Na Bwana na aongeze baraka Zake.

> *Na hii ndiyo* maana *iliyoandikwa, MENE, MENE, TEKELI, NA PERESI.*

12 Kama Maandiko yetu, asubuhi ya leo, yanaturudisha katika Agano la Kale, ili kuweka mawazo yetu kwa dakika chache zijazo kwenye tukio la kihistoria. Na tunajua kwamba historia hujirudia kila mara. Na katika somo langu sasa, ninasoma *Wazee Wa Kabla Ya Nikea*, na ninaweza kuona kupitia Maandiko, jinsi ambavyo tunarudia tena zama ambazo zimepita.

13 "Na Maandiko yote yametolewa kwa uvuvio." Na Bwana wetu mbarikiwa alisema, kwamba, "Maandiko hayawezi kuvunjwa. Maandiko yote lazima yatimie." Hiyo ni faraja iliyoje, kutupa sisi watu tunaosoma Maandiko hayo, tukijua kuwa tulichosoma hakiwezi kuvunjwa. Inatupa msingi thabiti zaidi kuweka imani yetu juu yake. Na kila Andiko lazima litimie.

14 Ndipo tunaona, ya kwamba katika kutimiza Maandiko, Neno ni kuu sana hata mara nyingi lina utimizo maradufu, na zaidi ya yote linajirudia angalau mara moja.

15 Kwa mfano, katika Biblia, katika Mathayo sura ya pili, Hilo—Hilo linasomeka, pale iliposema, "Kutoka Misri nimemwita mwanangu." Kama utasoma Maandiko hayo, na kufuatilia marejeo, utaliona huko nyuma, kwamba Mungu alimwita Mwanawe, Yakobo, kutoka katika Israeli . . . kutoka Misri. Na kisha pia inatimizwa tena wakati alipomwita Mwanawe, Yesu, kutoka Misri.

Nalo linaendelea tu kujirudia, kwa maana limevuviwa.

16 Ikiwa ningekuandikia barua, labda ungeithamini barua hiyo. Na kama ungeniandikia moja, nina hakika ningeithamini. Lakini barua yangu ingekuwa kwako tu. Kwa hivyo, baada ya kuisoma mara moja, unajua maana yote, na barua hiyo haingemfaa tena, mtu mwingine yeyote. Ilikusudiwa tu kwako; au yako kwangu.

17 Lakini sivyo ilivyo kwa Neno la Milele la Mungu. Limevuviwa. Kwa hiyo, ni kwa watu wote, katika nyakati zote, na kutimiza masharti yote. Hilo ndilo linalolifanya liendelee kujirudia. Historia inapozunguka, linazunguka na historia. Nalo halipotezi kamwe thamani Yake, kwa maana ni Neno la Milele la Mungu wa Milele. Haliwezi kupoteza thamani Yake.

18 Na tukio letu asubuhi ya leo liko Babeli. Ni vizuri sana kwetu kupata habari kidogo kuhusu jiji hili kubwa. Na nimekuwa nikisoma hivi majuzi juu ya Babeli, kutoka kwenye—kwenye . . . kijiografia ilipowekwa. Nami nilikuwa nikiisoma kutoka katika *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop, mojawapo ya historia za kale sana za Babeli.

19 Babeli inaonekana kwa mara ya kwanza mwanzoni mwa Biblia, kisha inaonekana katikati ya Biblia, na kisha inaonekana katika mwisho wa Biblia. Sababu inaanza katika Mwanzo ni kwa sababu Mwanzo ni sura ya mbegu ya Biblia. Hapo ndipo mbegu ya kila kitu kilicho duniani, leo, ilipoanzia, katika Babeli . . . katika Mwanzo. Samahani. Nayo Babeli ilianza katika Mwanzo.

20 Ilianzishwa kwanza na Nimrodi, ambaye alikuwa mwana wa Hamu. Na iliitwa kwanza, "Malango ya Paradiso." Kisha ikaitwa Babeli, nalo neno Babeli linamaanisha, "Iliyorudi nyuma."

21 Basi Nimrodi alianzisha huu katika mojawapo ya sehemu zenye rutuba zaidi za ulimwengu unaojulikana. Nao ulikuwa mji mkuu. Na ilianzishwa katika mabonde ya Shinari. Na Shinari ilikuwa . . . Bonde la Shinari lilikuwa mahali penye rutuba zaidi katika ulimwengu unaojulikana, kituo kikuu cha kilimo, na Mto mkuu Frati ukamwagilia maji mashamba yake. Tigri ulienea kaskazini, kwenye mlima, lakini Frati ulimwagilia maji Shinari. Na moja kwa moja katikati ya bonde hili, mji huu mkuu ulipandwa, nao ulikuwa ni mmojawapo wa miji mikubwa sana ya siku hizo. Palikuwa ni mahali mashuhuri, na palisheheni wanasayansi na akili ya ulimwengu unaojulikana.

22 Mji ulikuwa maili mia moja na ishirini kuuzunguka, kuuzunguka mji huo. Na kuta zilikuwa na upana wa futi mia mbili, na karibu urefu wa futi mia tatu. Ungeweza kuendesha magari sita ya farasi, kandokando, ukizunguka ukuta huu, na kukimbia kuzunguka ukuta.

23 Na halafu jiji hilo, pia, ndani yake, lilikuwa na mitaa yake mikubwa, mno. Na mitaa hii ilikuwa karibu sawa, au bora kuliko sawa, na mitaa ya kisasa ya leo. Ilikuwa na upana wa futi mia mbili. Hilo lilikuwa jambo geni kabisa kwa jiji la siku hizo, kwa sababu mitaa ilikuwa myembamba, kwa ajili ya gari dogo tu kupitia.

24 Wakati fulani uliopita, nilikuwa na majaliwa kuwa huko Oslo, Norway. Na chini kwenye sehemu ya kale ya mji, ambayo ina umri wa zaidi ya miaka elfu moja, ni vigumu kufinyilia gari lipite katika mitaa ya jiji, kwa sababu usafiri pekee waliokuwa nao ulikuwa ni magari ya vita au wapanda farasi. Na hivyo ndivyo maskini miji yote ya kale ilivyojengwa. Lakini Babeli hii ilikuwa na mitaa yenye upana wa futi mia mbili. Majeshi yangeweza kuandamana yakiwa yamevalia silaha kamili, na yote bega kwa bega, na upana wa futi mia mbili, gari baada ya gari.

25 Na ilijengwa kitu fulani kwa utaratibu wa Rumi, leo, ambapo Babeli ya kisasa inakaa. Kila barabara ilielekea kwenye makao makuu na kiti cha enzi, namaanisha, kiti cha enzi. Kiti cha enzi kilikuwa mahali pazuri katikati ya mji. Na mbele ya kiti cha enzi, mto mkubwa Frati unapita.

26 Na malango makubwa ya mji huu, upana wa futi mia mbili, na urefu wa futi mia na hamsini au mia mbili, uliotengenezwa kwa shaba thabiti.

27 Lo, lilikuwa jiji kubwa! Na katika kuta zake zote, lilikuwa na bustani kubwa zinazobembea. Na bustani hizi zilikuwa sehemu kubwa za burudani.

28 Na katika jiji hilo walikuwa wamekusudia kwamba wangeweza kuishi kwa njia yoyote ile waliyotaka kuishi. Kwa hiyo walifikiri, basi, kama wangeweza kufanya hivyo, wangejenga mnara mrefu sana, ili kama mafuriko ya maji ya

hukumu yakiwahi kuja, kwamba wangekimbia tu wapande juu ya mnara, nao wangekuwa salama.

29 Mnaona? Ni picha tu ya Marekani ya kisasa, kujaribu kupata sputniki ama kitu fulani, na kwenda mwezini, tukifikiri ya kwamba tutakuwa salama. Lakini Mungu anakuona, haijalishi mahali ulipo.

30 Na katika mji huu, walikuwa na kila aina ya mbinu za dhambi. Na mahali popote panapojiona kuwa salama, basi vurugu na uovu huingia. Walikuwa na wanasayansi bora kuliko wote ulimwenguni. Walikuwa na majeshi bora kuliko yote duniani. Walikuwa na magari bora kuliko yote ulimwenguni, watu waliofunzwa vizuri zaidi waliokuwepo. Na wanasayansi, na silaha zote, walikuwa wakuu. Walikuwa juu sana kuliko mataifa mengine. Nao, kwa kweli, mataifa mengine kwa namna fulani yaliwatazama, ama waliwainamia.

31 Na taifa linapoingia katika hali hiyo, basi wanafikiri wanaweza tu kufanya watakalo, na kupita nalo.

32 Lakini, kumbukeni, haidhuru kuta ni ndefu jinsi gani, Mungu hutazama chini kutoka Mbinguni. Na Mungu anachukia dhambi. Anampenda mwenye dhambi, lakini anachukia matendo yake, dhambi.

33 Na katika mji huu mkubwa, walikuwa waovu sana. Walifikiri, "Vema, tunaweza tu kufanya chochote tutakacho, kwa sababu hakuna kitu kinachoweza kutusumbua." Ikiwa hiyo si karibu tu picha ya taifa letu, leo, kumkataa tu Mungu!

34 Sasa, waliikataa rehema ya Mungu huko nyuma, pia. Walikuwa na nabii katika mji huo jina lake Danieli. Na ungeweza kuwazia mtu wa Mungu, akiona dhambi na hila, kama ilivyokuwa, alipiga kelele dhidi yake. Lakini walimcheka tu, kana kwamba wanafikiria, "Huyo mzee hajui anachozungumzia."

35 Na ndivyo ilivyo leo, kwamba watu wetu wa siku hizi wamekuwa hawamjali sana Mungu, mpaka tunahisi ya kwamba tunaweza kuishi tu jinsi tunavyotaka na kupita nayo. Lakini huwezi kufanya hivyo. Hutaweza kamwe kufanya hivyo. Mungu atahukumu dhambi.

36 Mtu fulani aliniambia, wakati fulani uliopita, alisema, "Mhubiri, msingi wetu wa Marekani ulijengwa juu ya sta—staha na heshima za wazee wetu. Walikuwa watu wa dini, kwa hiyo Mungu atalilinda taifa hili milele."

37 Hatakuwa na heshima zaidi kwetu kuliko alivyowafanyia Israeli. Israeli walikuwa watu Wake walioitwa na waliochaguliwa. Na walipopanda, walivuna walichopanda. Na hiyo huenda kwa watu binafsi. Haidhuru tunadai kuwa ni wa kanisa takatifu jinsi gani, au jinsi tunavyojaribu kuishi vyema,

Mungu anawajibika kwa Neno Lake, ili kutuhukumu kulingana na yale aliyosema.

38 Na nimetoa tamshi hili. Taifa hili likiepuka hukumu, Mungu atawajibika kufufua Sodoma na Gomora, na kuomba msamaha kwa kuwazamisha na kuwateketeza, kwa maana sisi ni waovu tu kama vile Sodoma na Gomora ilivyowahi kuwa. Na ikiwa aliizamisha Sodoma na Gomora, na kuwateketeza, kwa sababu ya dhambi yao, na asitutende sisi vivyo hivyo, basi atakuwa amewadhulumu na anastahili kuwaomba msamaha.

39 Haimbidi Mungu kumwomba msamaha mtu yeyote, au chochote. Dhambi itahukumiwa. Na itaadhibiwa, hakika tu kama vile kulivyo na Mungu Yule awezaye kufanya hukumu. Na hukumu ya Mungu ni takatifu. Mungu ni mtakatifu. Na, kwa hivyo, hukumu zake na kazi zake lazima ziwe za haki na takatifu, kwa sababu inakuwa Mungu mtakatifu, kwa ajili ya kazi Zake na hukumu Yake.

40 Na, loo, jinsi mji huu, unavyozagaa katika dhambi! Jinsi taifa letu, leo, linavyozagaa katika dhambi! Tunafikiri tu kwa sababu sisi ni Wapresbiteri, ama Wabaptisti, au Wapentekoste, ama chochote kile, hayo tu ndiyo Mungu anayohitaji. Anahitaji haki. Na hicho ndicho kitu pekee ambacho sheria yake itatambu-. . . kutambulika, ni haki. Yeye haliheshimu dhehebu.

41 Katika Kitabu cha Matendo, sura ya 10 na aya ya 35, nabii akasema, "Naona kwamba Mungu hana upendeleo wa taifa wala mtu, bali atawakubali wale watakaomtumikia kwa haki." Haijalishi unashiriki kanisa gani, Mungu anatarajia umheshimu. Na anataka umtumikie kwa haki. Tukishindwa kuwapelekea Injili, basi Mungu atawahukumu kulingana na maarifa waliyokuwa nayo, na jinsi walivyokuwa wanaheshimika Kwake.

42 Loo, Jina Lake libarikiwe! Kama unavyoweza kuhisi kwa urahisi, katika siku hii tunayoishi, jambo fulani liko karibu kutukia. Loo, ninatazamia kwa matarajio makubwa asubuhi fulani tukufu, kwa maana taabu zitakwisha, na Bwana mbarikiwa atakuja. Nasi tutanyakuliwa, kumlaki hewani. Loo, inapaswa kuwa nia hasa ya kila moyo, na lengo hasa la kila moyo, kuutazamia wakati huo, kuona ni lini shida na majaribu yetu yatakwisha. Na wakati . . .

43 Tunaelekeza mawazo yetu sasa Babeli, tena, kwa ajili ya kuendeleza Ujumbe wetu. Tunaona, katika mji huu mkuu, ya kwamba walipolindwa kabisa, hakuna taifa lingeweza kuwafikia. Mbona, walikuwa na kuta za futi mia mbili za kuchimba, mamia ya futi juu angani, na malango makubwa ya shaba ambayo ingechukua kundi la askari kulegeza. Walikuwa wamelindwa vyema. Hawakuwa na haja ya kuwa na wasiwasi na taifa lingine lolote. Sasa, sehemu hiyo ilikuwa sawa. Lakini

walipoweka dhambi mle, basi, kumbuka, Mungu anaweza kuangalia popote na kukuona, haidhuru umelindwa jinsi gani.

44 Pia ninataka kusema hivi. Kuna njia moja tu ya Mkristo kulindwa, hiyo ni, chini ya Damu ya Mwana wa Mungu aliye hai. Hicho ni kitu kimoja ambacho hawezi kukitazama na kukihukumu. Ikiwa umefunikwa na Damu, basi Mungu hatakuona. Alisema, katika Maandiko, "Nionapo damu, nitapita. Nitapita juu yako."

45 Lakini watu hawa hawakujali kuhusu hilo. Walikuwa na dini zao wenyewe, kwa hiyo waliishi kulingana nazo. Wajua, "Iko njia ionekanayo kuwa sahihi machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti."

46 Sasa, katika jiji hili, walikuwa na mfalme ambaye alikuwa mmoja wa hawa wavulana wa siku hizi wachangamfu, loo, kitu kama baadhi ya wachekeshaji wetu wa redio, Arthur Godfrey wa kisasa, ama Elvis Presley, ama mtu kama huyo. Loo, alikuwa mvulana maarufu, wa burudani. Naye alipenda burudani zake, kwa hiyo alikuwa anaenda kuwafanyia watu wake wote karamu ndogo ya roki.

47 Loo, ikiwa hiyo haikuwa laana! Na kuwazia ya kwamba wanaume na wanawake, wanaojiita watumishi wa Kristo, wanajiingiza katika mambo kama hayo, santuri katika nyumba zao, kwenye mashine zao. Tupa vitu hivyo nje ya mlango!

48 Na huyu jamaa akawazia, "Vema, sasa, tutakuwa na wakati mzuri sana." Naye akatuma mwaliko mkubwa kwa watu mashuhuri wote. Alichagua wateule wake, wale ambao wangeweza kucheza vizuri zaidi, na wanawake ambao walikuwa warembo zaidi. Naye akawaleta wote kwenye bustani kubwa inayobembea, nyuma tu ya ikulu, kwa ajili ya dansi ya kisasa. Na walikuwa wanaenda kuwa na burudani nyingi. Na askari wote, na wote, wakalewa sana. Ikiwa hiyo si Marekani ya kisasa, sijui iko wapi. Kwa hiyo walikuwa na wakati mzuri. Basi wakawasha mapambo yote, kama tu kipindi kizuri cha runinga.

49 Nao walikuwa kule nyuma, wanawake, bila shaka, wakiwa na walezi wa watoto nyumbani, wakiwatunza watoto wao wachanga. Nayo Biblia ilisema, "Akawaita masuria wake wote." Na *suria* alikuwa "kahaba" halali. Na tofauti pekee ni, wa leo, wangali ni kitu kile kile, lakini si halali. Na waliwaacha watoto wao nyumbani na walezi, nao wakavaa nguo zao mpya, za kisasa, sketi zao ndogondogo na kadhalika. Nao wakaenda kwenye sherehe ya mfalme, au karamu ya roki.

50 Loo, hivi hamwezi kuona Marekani mahali pale pale? "Loo, mfalme aliidhinisha, kwa hiyo lazima iwe sawa. Mfalme akifanya hivyo, vema, hilo latosha." Vema, kwa sababu tu Marekani inakuruhusu kuuza wiski, sigara, na tumbaku, na bia, hilo halilifanyi kuwa sahihi, machoni pa Mungu. Mungu atahukumu dhambi. Unasema, "Vema, taifa letu linaiuza."

Lakini unapaswa kuwa na kanuni halisi ya mwanamume na mwanamke, na ujiepushe nayo. Taifa letu linatawaliwa na ibilisi, kama mataifa mengine yote. Biblia inasema yanatawaliwa. Kwa hivyo huwezi kwenda kwa namna ta—taifa linavyotawaliwa.

51 Shetani alisema, "Falme hizi zote ni zangu. Nitafanya nazo kile ninachotaka." Naye akamwambia Yesu, "Nitakupa Wewe kama utaniabudu."

52 Yesu alijua atazirithi, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, hivyo akasema, "Imeandikwa, 'Utamwabudu Bwana Mungu wako, na kumtumikia Yeye peke yake.'" Hayo ni mahubiri mazuri kwa kanisa, achilia mbali kwa Shetani. Haijalishi una nini, tumeamriwa kumwabudu Bwana Mungu wetu, na Yeye pekee ndiye tutamtumikia.

53 Basi mfalme akaandaa karamu kubwa. Naye akatayarisha chakula chote, na bia zao bora zaidi, na divai zao. Zilizotangazwa vizuri zaidi, walizokuwa nazo. Naye alikuwa anaenda kuwa na wakati mzuri sana. Naye akawaalika wasichana wote wa Hollywood, na wote hao. Nao wote wakaja, na wacheza densi bora zaidi waliokuwa nao. Wote walikuwa katika bustani hii kubwa huko nje, wenyewe wakiwa na roki ya kisasa. Wakati wa jinsi gani! Kucheza, kunywa, kuwa na burudani!

54 Je, Biblia haisemi yangekuwa hivyo? Kasema, "Watakuwa wakaidi, wapenda makuu, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasiojizuia, wakali, na wanaodharau wale walio sawa na Mungu." Siku ya jinsi gani tunayoishi! Sasa nataka uchune dhamiri yako ya kiroho.

55 Ilikuwa ni katika wakati huu, wakati wao walikuwa na haya yote, na. . . Naweza tu kuona wa—wasichana na bia zao, wakinywa. Na walikuwa wakifanya ro—roki yao, ama bugi-wugi, wakiwa na wakati mzuri tu huko, wakicheza dansi huku na huko. Na hao askari walevi wakiwazungusha hao wanawake huku na huko, na kuwavuta karibu nao, na kuwaweka kwenye mapaja yao. "Na walikuwa tu na maskini burudani safi." Hiyo ndiyo Amerika inaiita leo, "Burudani safi kidogo tu." Ni dhambi!

56 Biblia ilisema, "Mwanamke anayeishi kwa anasa amekufa hali yu hai." Na jinsi wanawake wetu wa Marekani wamepoteza maadili yao, hata hawajui neno *maadili* linamaanisha nini.

57 Nami nilikuwa nikiwafuatilia, kuhusu hilo, si muda mrefu uliopita. Ndipo mwanamke mmoja akaniambia. . . Nilimwambia. Nilisema, "Unavaa nguo jinsi unavyofanya, itakubidi kujibu Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi." Alikuwa mwanamke aliyeolewa.

58 Akasema, "Nitakupa kuelewa, Ndugu Branham, ya kwamba sijafanya jambo lolote baya."

59 Nikasema, "Lakini je, yule mtu mwingine aliyekutazama amefanya kosa lolote? Kwa maana Yesu alisema, 'Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini na yeye tayari moyoni mwake.' Basi mwenye dhambi huyo atakapojibu kwa uzinzi, utajibu kama mwenye hatia, kwa kuwa ulijianika kwake namna hiyo."

60 Akasema, "Vema, Ndugu Branham, wanauza aina hiyo ya nguo. Hiyo ndiyo aina pekee wanayouza."

61 Bado wanauza cherehani. Bado wana vitambaa. Ni aibu kuona vile, wanawake wetu wa siku hizi. Enyi wanawake wa Kipentekoste, ni aibu iliyoje!

62 Na wewe mwanamume, wewe mwanamume wa Kipentekoste, ambaye utamwacha mwanamke wako atende hivyo, hilo linaonyesha kwamba wewe ni mwanamume kiasi gani hasa. Unapaswa kuwa ndiye kichwa cha nyumba. Loo, ni aibu iliyoje!

63 Unasema, vema, mke wako anavuta sigara. Ni nini kilimwingiza katika hilo kwa kuanzia? Yeye ana makosa katika kuifanya. Anajitia sumu. Anawatia watoto wako sumu. Anailaani familia nzima. Na aibu kwa Kanisa la Mungu aliye hai!

64 Na ninyi mnaowaacha watoto wenu, wasichana wenu wadogo, watoke na hawa wavulana wanaotembea hapa katika takataka hizi za roki ya kisasa. Aibu kwenu, mama na baba! Unasema, "Naam, wanafanya tu watakavyo." Bado unayo makasia.

65 Nina wawili huko juu. Sijui watakuwaje. Lakini ikiwa mzee huyu, Branham, ataishi muda mrefu vya kutosha na kuwa na akili timamu, wanaweza kwenda lakini watakuwa wamejaa malengelenge wakiwa huko.

66 Ni aibu! Kuna watoto haramu zaidi wanaozaliwa ulimwenguni leo, Marekani. Kila mwaka hutoa watoto haramu zaidi kuliko vita vilivyotoa katika miaka minne ya mauaji. Loo, ni ishara kuu ya wakati wa mwisho! Hakika ndivyo.

67 Sasa nataka umtambue mfalme huyu. Loo, alikuwa mtu mashuhuri. Loo, alikuwa Arthur Godfrey mzuri, pamoja na vichekesho vyake vyote vichafu.

68 Na ninyi wanawake mnaobaki nyumbani, badala ya kuchukua wakati wenu kwa ajili ya mikutano ya maombi a—asubuhi, unafungua mkorofi kama huyo na kumsikiliza, halafu unajiita Mkristo. Anafanya nini ila kulala chini pale pamoja na hao wasichana, na kadhalika! Mbona, yeye ndiye aibu kubwa zaidi ambayo taifa hili limewahi kuwa nayo. Loo, ndiyo, "Yeye ni Mmarekani halisi." Ukiita huyo Mmarekani, ni. . . Anaweza kuwa Mmarekani mzuri, lakini ni mbali sana na Ukristo. Lakini

huna wakati kwa ajili ya mkutano wa maombi au kusoma Biblia. Sasa unaona mahali tulipo?

69 Wale wanawake, wale masuria waliokuwa pale pamoja na mfalme usiku ule, kama wangemsikiliza Danieli, hawangekuwa hapo.

70 Lakini angalia karamu ikiendelea, unajua, na wote walipata joto sana, pamoja na divai zao nzuri na wiski na bia, waliyokuwa nayo. Na kisha wakasema, "Hebu tujiburudishe." Loo, naam, huyu Arthur Godfrey wa kisasa alitaka kutoa moja kuhusu yule mhubiri mwenye upara, ama chochote kile, mwajua. Hivyo akasema, "Tutakwenda kuchukua vyombo vya nyumba ya Mungu wao, na tutakuwa na mzaha kidogo." Ikiwa huo sio mzaha mkubwa kwenye redio au televisheni, sijawahi kuona mmoja.

71 Unaona, mtu huyo anakufa, lakini roho inaendelea kuishi. "Loo, tutamwambia mmoja tu kuhusu *hili, lile,* ama *linginelo*, kuwa na mzaha mzuri." Hapa niliwasikia hivi majuzi, kwenye redio, wakiimba *Watakatifu Watakapokuwa Wakiingia,* kwenye taarabu; *Nionapo Damu,* kwenye bugi-wugi. Ni fedheha iliyoje! Je, unafikiri Mungu mtakatifu anaweza kusikiliza hayo, na kuwa mwenye haki na asihukumu?

72 "Lakini tumelindwa! Sisi ni taifa kubwa. Sisi ndio wakuu kuliko wote ulimwenguni!" Ndivyo walivyokuwa. Lakini kulifanyika nini?

73 Kasema, "Nenda kachukue vyombo hivyo tuwe na wakati mzuri." Nao wakaenda na kuvichukua vyombo vya Bwana, vile vitu vitakatifu.

74 Ambavyo, "Wewe ni chombo cha Bwana." Wewe ni chombo cha Mungu, ambapo anamimina Roho Wake Mtakatifu.

75 Nao wakasema, "Hebu tuwafanyie vichekesho kidogo, mtakatifu anayejibingirisha." Kwa hiyo wanakwenda na kukichukua, na kujaza sahani zao, ama ninii zao . . . vitu, kwa—kwa mvinyo. Na halafu huyu Arthur Godfrey wa kisasa, wakati wasichana walipokuwa wameketi kwenye mapaja ya askari, na kutengeneza "whoopee," na kuwa na wakati mzuri, na—na kucheza kwao na kuendelea. Na labda mume nyumbani, analea mtoto; na labda mwa—mwanamke nyumbani, analea mtoto, na mume wake mlevi kule juu; karibu nusu na nusu tu.

76 Na hapo walikuwa, wakati huu wote mkuu, wamelindwa vyema, hakuna kitu kinachoweza kuwasumbua. Hakika! Taifa kuu kuliko yote chini ya mbingu, walikuwa. Wanasayansi wote mashuhuri walikuwa katika ulimwengu wao. Zana zote mashuhuri za vita zilikuwa chini ya mamlaka yao. Walikuwa nyuma ya kuta, hivyo hakuna kitu kingeweza kuwasumbua. Walikuwa na wakati mzuri.

Hawakujua kwamba Mungu angeweza kutazama chini awaone.

77 Na huko katika hilo, mfalme huyu wa kisasa na vichekesho vyake vya Elvis Presley, na kuimba, labda walikuwa wanazifurahia sana. Hivyo akasema, "Waleteni hao watakatifu wanaojibingirisha na tuburudike." Basi akamimina divai katika chombo, akawa anakunywa, akisema, "Loo, hiyo ni nzuri!" Mapambo yote! Na wote, "Naam, hiyo ni nzuri!"

78 Kama tu Marekani siku hizi, pamoja na baadhi ya vichekesho vyao vichafu, na kadhalika, walivyo navyo kwenye televisheni na redio. Na katika ninii yao ya kisasa...Na ninyi watu mnaojiita Wakristo, mkisikiliza upuuzi kama huo, sasa mnaweza kuona tunaposimama. Ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, na Mpresbiteri, ninyi Wapentekoste wazuri, jambo fulani liliwapata. Shauku zenu zimekuwa mbaya, kwa maana kile kilicho moyoni mwako utafanya. Usingeweza kufanya...

79 Haitakuwa jambo la kushangaza sana kwangu, kuona nguruwe kwenye lundo la mbolea, akila. Hiyo ndiyo asili yake. Lakini hakika ingenishangaza...Sijapata kuona, na kamwe sitaona, mwana-kondoo akila pamoja naye, kwa sababu asili ndani yake ni tofauti.

80 Huwaoni Wakristo wakifanya mambo hayo. Asili yao, asili ya Roho Mtakatifu mkuu, haitawaruhusu kufanya mambo hayo. Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia, ama mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Sasa mnaweza kujihukumu wenyewe, la sivyo Neno linawahukumu. Ukipenda mambo hayo, upendo wa Mungu umeondoka kwako.

81 Mungu ana nafasi ya kwanza au hana nafasi. Jina Lake lihimidiwe! Nimefurahia sana hilo. Nina furaha sana kwamba Yeye ni safi na mtakatifu. Tunaweza kumtumainia Yeye. Hapatani na chochote. Yeye ni Mungu, na Mungu peke yake. Sio...Hatashuka kwetu; hatuna budi kuimarika tujifananishe na Yeye. Haimpasi kuja kwa mawazo yetu; inatupasa kuimarika tutoshee mawazo Yake. Hatasikiliza amri zetu; tunaenda kusikiliza amri Zake.

82 Lakini, bila shaka, tunaweza kufanya tu kile tutakacho. Nami nasema hili kwa heshima. Asilimia tisini ya wachungaji, wamekuwa wanyonge sana, hawatahubiri dhidi yake. Ni tiketi ya posho kwao. Afadhali nipate chakula kwa shida, na kuvaa magunia ya nyasi kufunika uchi wangu, na kuhubiri Injili, Kweli, kuliko kuwa na kuku wa kukaanga mara tatu kwa siku na kupatana na takataka za shetani. Ninakuwa mzee; nami nilimtetea nilipokuwa kijana. Ninataka kusimama hodari zaidi sasa, kwa maana naona saa imekaribia. Je, unafikiri manabii wa Agano la Kale wangefanya nini kama wangefufuka leo? Angalia masharti!

83 Na jamaa huyu akiwa ameinua chupa yake ya divai, akinywa, akiwa na wakati mzuri. Alisema, “Dakika moja tu. Nyote, ninyi, nyote mnisikilize. Fungueni redio zenu sasa.”

84 Mambo ya kishenzi, machafu na ya kinyaa ambayo yanaruhusiwa, programu ambazo hazijadhibitiwa! Ilianza lini? Angalia nyuma kupitia historia. Ilianza kule nyuma katika siku za Clara Bow. Na wakati huyu Mteksas mwovu, mwenye njama alipoenda huko nje na kutengeneza nguo za ndani za wanawake hawa zilizowafanya waonekane wa kuvutia kingono, na hili likaanza. Wimbo wa kwanza wa uchafu waliouacha upite, ulikuwa juu ya wanawake kuteremsha soksi zao na kuonyesha magoti yao mazuri. Walipita na huo, na sasa haujadhibitiwa. Wanaweza kusema na kufanya kile watakacho. Ibilisi amechukua kitu hicho bila kufyatua risasi. Hiyo ni kweli. Unafikiri hao makahaba wa Hollywood, walioko kuzimuni, leo, wangefanya nini kama wangeweza kurudi? Wangeifanya kuwa tofauti. Lakini ushawishi wao juu ya ulimwengu umeweka ulimwengu katika moto wa uharibifu.

85 Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Ushawishi wa Kanisa la Kikristo unapaswa kufanya nini? Kuutia moto ulimwengu kwa Ukristo! Lakini, badala ya hayo, tunajaribu kujifananisha nao. Kristo ndiye mfano wetu, na si bingwa fulani wa Hollywood, au bingwa fulani wa televisheni.

86 Lakini sisi ni wa kisasa. Tunavuta Pall Mall, na utaenda kuzimu kwa kufanya hivyo. Picha za wasichana hapa nje, wakiwa na sigara, wanawake wenye sura nzuri, huo ni udanganyifu wa ibilisi. Mwangalie, miaka michache baada ya kuvuta sigara, akiwa na TB, amelala kule, akifa, mnyonge. Lakini ni ya kisasa. Wanaweza kuiweka mbele ya vijana.

87 Nawe ukiweka picha ya uponyaji wa Kiungu, ama chochote kile, ama cha Kristo, hawatakuruhusu kufanya jambo hilo.

88 Lakini sisi ni wa kisasa. Hatuna budi kwenda kama ulimwengu wote. Ishara zote kuu za bia, Oertel’s ’92, na Pabst Blue Ribbon’s, na hizo zote. Wanafanya nini? Wanaiweka kwenye vipindi hivyo vya televisheni kwa sababu haitozwi kodi. Ibilisi ameifanya hivyo.

89 Ee Mungu, uturehemu. Je, hamwoni, jamani, tuko mwisho wa barabara?

90 Jinsi ibilisi amejiingiza kwenye mambo hayo. Ameiruhusu kwa sababu anajua siku zake zimehesabiwa.

91 Kwa hivyo kijana huyu na bilauri yake ya divai, akiiinamisha kwa kupongezana. Loo, jamani! Ningewazia wanaume wote walitaka kutenda kama yeye.

92 Waone wavulana wadogo huko shuleni, inapowabidi kuvuta maskini ovaroli zao kwenye makalio yao, na kuziacha nywele zao zikue kama kundi la majangili, kutenda kama Elvis Presley.

93 Mungu ambariki yule mkuu wa chuo kile hivi majuzi, aliyesema, "Utanyooka na kuvaa kama mwanaume, au utatoka katika chuo hiki." Huyo ni Mmarekani halisi. Alisema, "Wanapovalia hivyo, wanafanya hivyo." Na hiyo ni kweli.

94 Na unapovalia kama kahaba, utatenda kama mmoja. Loo, una mengi ya kufanya, ni aina gani ya roho iliyo ndani yako. Hakika. Inakufanya utende kile kilicho ndani yako. Inakufanya uvae, na kutenda, na kuishi. Chochote kilicho ndani yako, kinakutawala. Hakika.

95 Lakini sasa ameinua bilauri yake. Loo, jinsi alivyokuwa tu katika tabasamu lake kuu, densi yake ya kutikisa mwili ambayo alikuwa anaenda kufanya mbele ya watu wote. Hicho si kipindi kizuri cha televisheni? Hivi—hivi Hollywood isingeendea kitendo hicho? "Loo, nakuambia," anasema, "hili hapa tutakalofanya. Unajua kundi lile la watakatifu wanaojibingirisha tuliokuwa nao hapa?" Unaona?

96 Na karibu tu wakati alipoanza kunywa, alitazama ukutani. Unajua, kwenye bustani, kulikuwa na vinara vikubwa vya taa vilivyotundikwa. Na kulikuwa na plasta ukutani. Na taa zilikuwa zinaakisi dhidi ya plasta hii, kutoka kwenye bustani. Na macho yake yakatokeza. Na kweli alishtuka sana. Biblia ilisema alishtuka, ilisema ya kwamba, "Mifupa yake ilitenguka, nayo ikagongana."

97 Ndiyo, na baadhi ya siku hizi, taifa hili litatikiswa kabisa, hakika vya kutosha. Loo, naam. Hakika.

98 Walisema, "Hao watakatifu wanaojibingirisha, hao waponyaji wa Kiungu, *hawa, hao,* na *wengineo,*" kile wote walicho. Subiri tu. Mungu ni mwenye haki.

99 Yeye atatuma Ujumbe, hata hivyo. Alifanya hivyo katika nyakati zingine zote. Atafanya sasa. Naye anafanya jambo hilo, na uamsho unakaribia tu kwisha. Mnakumbuka, ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Nilisema, "Marekani ilifanya uamuzi wake wa mwisho mnamo 1946." Tazama tangu wakati huo. Amekwisha. Na hakuna kilichobaki isipokuwa hukumu na machafuko. Angalia kile kilichotokea kwa muda huo. Iangalie tu, jinsi itakavyoenda haraka zaidi na zaidi. Tuko mwisho. Tunaishi katika vivuli vya Kuja Kwake.

100 "Na kutakuwa na ishara mbinguni juu na duniani. Mioyo ya watu ikizimia; hofu, wasiwasi wa wakati; dhiki kati ya mataifa." "Jinsi watu watakavyokuwa wakaidi, wenye kujivuna!" "Jinsi binti za Sayuni, kanisa, wangeenenda kwa majivuno, kujikweza; pamoja na vile angetembea, na kuliza njuga na kujipinda akitembea."

101 Tuko wapi? Tuko pamoja na karamu kubwa ya muziki wa roki ya Belteshaza. Na kanisa limenaswa kwenye wimbi, kupitia televisheni, kupitia redio, kupitia Hollywood. Na hapo ndipo tulipo. Wanawake wa Kikristo wa kweli wakikata nywele

zao, wakijipodoa nyusoni, wakivaa maskini nguo za kizinifu, kwa sababu watu waliopotoka wamewaambia hakuna ubaya katika hilo.

102 Mwanamke Mkristo, mhubiri, alimtuma msichana hapa chini hivi majuzi, alionekana kana kwamba alimiminwa ndani ya nguo zake. Alisema, "Loo, Ndugu Branham, wewe ni wa mtazamo wa kale. Mchungaji wetu huwakomboa wanawake."

Nikasema, "Kuwakomboa kutoka kwa nini?"

103 Wanawaweka huru kutoka kwa Kristo na adabu ya kawaida. Loo, mwanamke ni maarufu sana. Hakika. Lakini chochote kinachofanya hivyo ni mtoto wa kuzimu. "Kwa matunda yao mtawatambua." Ni siku ya jinsi gani tunayoishi! Hakika. Siamini . . . najua inasema jinsi vile, unavaa nguo za aina gani, na kadhalika. Lakini, mwanamke, hivi unatambua unachofanya? Unajifanya kuwa alama ya ngono kwa maskini kila mhuni anayepita karibu. Lakini unataka ukombozi. Inaonyesha ni roho gani iliyo ndani yako. Unataka kuwa huru kutoka kwa Kanisa, huru kutoka kwa Kristo, huru kutoka kwa Roho Mtakatifu, ili uweze kuishi kama hao wengine. Hilo haliachi nje Maskani ya Branham. Hiyo inajumuisha Maskani ya Branham, yote! "Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Sisi hapa. Loo, siku ya jinsi gani! Wakati wa jinsi gani!

104 Naye amevurugika kabisa. Naye akatazama, na kando ya ukuta palikuwa na sehemu ya mkono wa Mwanadamu. Nao ulikuwa ukiandika ukutani, "MENE, MENE, TEKEL, NA PERESI."

105 Loo, wote wanaanza kumtazama Godfrey huyu wa kisasa ambaye alikuwa na umaarufu mkubwa. Ana shida gani? Amevurugika kabisa, hakika kabisa. Amesimama . . . Biblia ilisema, "Magoti yake yalikuwa yakigongana." Na jambo fulani lilikuwa limetokea. Nini? Hakuweza kuelewa. Alifikiri hakuna mtu angeweza kumfikia.

106 Lakini Mungu anaweza kukufikia, haijalishi mahali ulipo. Anakujua. Anazijua kazi zako.

107 Kwa hiyo anasema, "Kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni, kumwita mchungaji." Kwa hiyo akaenda na kumwita mchungaji, na kadinali, askofu mkuu, na mapapa wa kanisa lake. Akawaleta wote ndani. Akasema, "Hii ina maana gani?" Sasa utaiona Marekani ya kisasa. Hawakujua lolote kuhusu mambo ya kimbinguni, kwa hiyo hawakuweza kuyaelewa.

Jina la Bwana libarikiwe!

108 Ungeweza kutilia shaka, basi, kama wangemwita Roho wa Mungu aliye hai, "Mpiga ramli, au shetani"? Hawajui lolote kuhusu mambo ya kimbinguni. Wote wamefungwa katika madhehebu yao. Hawajui lolote juu Yake. Wanasema, "Loo, hiyo

ni telepathia ndogo tu ya kiakili." Lakini mwandiko wa mkono uko ukutani.

109 Alifanya ishara hiyo mbele ya Myahudi, kwa kuifunga yao. Alifanya hivyo mbele ya Wasamaria, lakini si Mmataifa. Kwa nini? Ilimbidi kungoja hadi dhambi za Waamori zilipolundikana.

110 Sasa maandiko ya mkono yako ukutani, kwa ajili yetu. Wanafanya nini? Je, wanaisikiliza? Hapana, bwana. Wanaendelea tu na Arthur Godfrey, na Elvis Presley, na Pat Boone, na wengine wote. Vijana wa kisasa, matineja, vurugu, hivyo ndivyo ilivyokuwa kule, hasa.

111 Akawaleta wachungaji wote ndani, wakasema, "Vema, sisi, hatujui Hilo. Labda . . . Loo, hilo labda ni kivuli mahali fulani."

112 Mfalme alikuwa na akili nzuri kuliko hiyo. Naye akasema, "Nitampa mtu yeyote sehemu ya ufalme wangu, nami nitamvisha, na nitaweka mkufu wa dhahabu shingoni mwake, kama anaweza kulifasiri Hilo." Lakini hawakuwa na kipawa cha kutafsiri. Hawakujua lolote kulihusu. Waliamini siku za miujiza zimepita.

113 Je, hao si ni wahubiri wetu wa kisasa? Je, hao si ni waangalizi wetu wakuu, maaskofu wetu? Hawajui lolote kuhusu mambo ya kimbinguni. Hiyo ndiyo sababu wangeweza kumwita Roho wa Mungu aliye hai, "Uigizaji; kujifanya."

114 Ee Mungu, kirehemu kizazi cha uzinzi na kichafu kinachoangamia kutoka katika uso wa dunia.

115 Huyo hapo. Bado anagonganisha magoti yake. Kulikuwa na shida. Alijua kulikuwa na kasoro fulani. Loo, kulikuwa na ishara ya kimbinguni. "Iliingiaje humu? Ilitoka wapi?" Ilitoka Juu. Ikashuka, ambapo hapakuwa na kuta. Ingeweza kuingia.

116 Na, leo, tumecheza roki. Tumewapeleka watoto wetu kwenye televisheni na vipindi visivyodhibitiwa. Tumeruhusu sakafu zetu na meza zetu kujaa hadithi chafu za zamani za mapenzi, badala ya Neno la Mungu. Hakuna mtoto katika jiji hili, ila ajuaye zaidi kuhusu Arthur Godfrey, au Elvis Presley, au Pat Boone, au David Crockett, kuliko wanavyojua kuhusu Yesu Kristo. Hiyo ni wazi, lakini, loo, ni kweli kabisa.

117 Si ajabu kuna kuanguka! Na wachungaji wanajua nini? Hawajui sababu yake ni nini. Wao ndio sababu yake.

118 Naye huyo alikuwa amesimama; ndivyo Belteshaza alivyoisababisha, kuuacha ufalme wake ufikie mahali kama hapo.

119 Na, leo, katika mambo haya yote tunayopitia, tulifikiri tumeimarishwa. Tunafikiri, "Sisi ndio taifa bora na mashuhuri kuliko yote duniani. Tunayo sayansi yote hapa."

120 Naye Belteshaza hakujua, ya kwamba hakuwa na wanasayansi wote. Kulikuwa na taifa linaloitwa "Wamedi na Waajemi," walikuwa na kazi fulani ya kisayansi, pia (Ambao sasa ni Wamedi na Waajemi, ama Wahindi, Wahindu katika India, kama vile ndugu yetu alivyonena hivi punde; hatimaye walikwenda, wakaishia huko India, kama Wahindu, Wamedi na Waajemi.), na walikuwa wameipata kisayansi njia ambayo wangeweza kuukwepa mto Frati. Hawakuweza kupita kwenye kuta, lakini waliupita mto, na walikuwa wakija chini ya malango. Sayansi inafanya kazi mahali fulani. Taifa kubwa, la kikafikiri na lisilo la kitauwa wakati huo, na Mungu akaweka ishara ukutani, ili wajue kwamba siku zao zimetimia.

121 Na Mungu ameweka ishara kwenye ukuta wetu na karamu yetu kuu ya roki, na kuna sputniki inayoruka angani. Loo, tulifikiri tulikuwa nayo yote, sivyo? Tulifikiri tulijua yote. Lakini Urusi, kulingana na sayansi yetu wenyewe, wako miaka mitano mbele yetu. Na tutakapotwaliwa, katika miaka mitano, watakuwa miaka kumi mbali zaidi. Mungu anaruhusu taifa lisilo la kitauwa, akiwaacha watu wasio watauwa waliowachukua wanasayansi hao wa Kiyahudi kule juu, na wako mbali sana mbele yetu. Tunaweka wakati wetu kwa mvinyo, wanawake, na burudani. Nao wanafanya kazi mchana na usiku, jinsi ya kutulipua. Hakuna jambo moja ambalo linaweza kuwazuia kuifanya hivi sasa. Angalia, hali tuliyomo, taifa zima.

122 Unamkumbuka yule afisa wa jeshi? Mimi na Ndugu Roberson tulikuwa tunazungumza jana. Walimhoji, mmoja wa wanasayansi mashuhuri. Akasema, "Sitaki uwaogopeshe watu, lakini nataka utuambie ukweli. Je, kuna hatari?"

"Dakika yoyote inaweza kutokea."

123 Jambo pekee, tunadanganyana tu. Tukawasha kombora letu dogo, nalo likatoka nje, futi tatu kutoka ardhini. Sasa tunainua lingine, nalo linayumba. Kwa nini? Tumezitia sumu akili zetu kwa sigara, na wanawake, na wiski, na burudani, na haimpendezi Mungu wa Mbinguni. Nayo Maandiko yanatabiri ya kwamba Urusi itafanya jambo hilo. Tuko wapi? Tuko mwisho. Kila taifa linaogopa sana. Ninaamini ya kwamba wangeweza kuweka kombora, sasa hivi, na kuangamiza taifa zima. Katika muda wa dakika tano, angekuwa si chochote ila unga, na kurudi kwenye gesi ambazo ulikuwa hapo mwanzo. Wanaweza kufanya hivyo.

124 Loo, tumekuwa na karamu ya muziki wa roki. Tumemsahau Mungu. Tumefuata sana televisheni, tukafuata sana ulimwengu. Na wamekuwa wakijiandaa wakati wote, kama tu Wamedi na Waajemi. Na sasa ya kimbinguni yamekuja, na maandiko ya mkono yako ukutani; sio ukutani, bali angani. Na sasa sote tumeshtuka. Loo, naam. Sayansi yetu ya kisasa imetikisika.

Taifa letu limetikisika. Inaweza kutokea kabla ya ibada hii kumalizika.

125 Lakini nataka uone mwingine. Nataka ukumbuke kwamba walipokuwa bado katika hali hiyo, chini ya shamrashamra za ulevi, kulikuwa na malkia mdogo. Hakuwa kwenye karamu ya roki. Hapana shaka alikuwa akisoma unabii wa Danieli. Hakuwa akijiingiza katika dhambi zao. Naye akaja mbio. Wakati mfalme hakujua la kufanya, alikuja mbio. Naye akasema, "Ee mfalme, uishi milele! Najua nyote mmeshtuka. Nyote mnafadhaika. Na mchungaji wenu, na hakuna hata mmoja wa washauri wenu, papa wenu, na makadinali wenu, na watu wenu wa wilaya, na wasimamizi wenu, hakuna hata mmoja wao anayeweza kuwatafsiria. Lakini kuna mtu, kuna mtu katika ufalme wako, anajua mambo ya kimbinguni."

126 Loo, Jina Lake libarikiwe! Kanisa, kuna Mtu katikati yetu, leo. Anaweza kusoma ya kimbinguni, na anaweza kuandika ya kimbinguni. Kuna Mtu. Loo, ninatumaini ya kwamba utakutana Naye. Ninatumaini ya kwamba ataingia moyoni mwako sasa hivi. Atazungumza nanyi wanawake. Atazungumza na ninii yenu. . .ninyi wanaume, na atawaruhusu kuona hali ambayo mmeingia. Yeye Ndiye pekee ambaye anaweza kusoma hali yako.

127 Ningeweza kuhubiri mpaka sauti yangu isiwepo tena. Ningeweza kulia hadi machozi yanichome yakitiririka mashavuni mwangu. Haingefaa kitu, kwa sababu mimi ni mwanadamu tu.

128 Lakini kuna Mtu. Jina Lake ni Yesu. Anaweza kukuambia *Hii* inamaanisha nini. Je, hutaponyoka na kuzungumza Naye kidogo tu?

129 Nini maana ya sputniki hizi angani? Kuna nini? Babeli hii ya kisasa ni nini, ambayo tunajaribu kutengeneza mashine ya kutupeleka mwezini? Hutaweza kamwe. Inahusu nini? Sayansi haijui. Wako katika mbio za kiwazimu kutafuta kitu fulani, na hawajui ni nini.

130 Lakini kuna Mtu. Kuna Mtu ambaye anajua kwamba yote inahusu nini. Yeye Ndiye aliyeiandika *Hapa*. Anajua jinsi ya kusoma Neno hili. Loo, Yeye anajua maana Yake, kwa kuwa Yeye ana BWANA ASEMA HIVI. Aliahidi hilo. "Kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya. Ikiwa wataniita Mimi, 'Beelzebuli,' mkuu wa nyumba, ni zaidi sana vipi watawaita wa nyumba Yake!"

131 Maandiko ya mkono yako ukutani; sputniki angani. "Matetemeko makubwa ya ardhi kila mahali; volkano zinakuja; mawimbi ya maji yanavunja fuo." Ni nini? Maandiko ya mkono. Sio tu angani, bali duniani. "Kutakuwa na ishara mbinguni na duniani. Moyo wa watu ukizimia."

"Loo, hatujui la kufanya."

132 "Kuchanganyikiwa kwa wakati; dhiki." Dhiki ni nini? Dhiki kati ya mataifa, yote hayo. Acha tu kombora moja liruke, hilo latosha. Ni nini?

133 "Kuna mtu anayeweza kuitafsiri." Alikwenda na kumleta mtu huyu.

134 Mungu nipe nguvu asubuhi ya leo, Mungu nipe uwezo; ili kumleta Mtu huyo kwenye hitaji lako leo, nimlete kwako. Yeye Ndiye anayeweza kuifasiri kesi yako. Yeye Ndiye anayeweza kukuambia ni wapi ulifanyia kosa lako. Anaweza. Ndiye anayeweza kukuambia ulipoenda kombo. Yeye Ndiye anayeweza kukuambia mahali pa kuanzia.

135 Naye akaenda akamchukua Danieli, mwakilishi wa Mungu. Naye akapanda juu.

136 Unaweza kuwazia nabii mtakatifu akisema, "Ee mfalme, nina heshima kuwa hapa. Loo, nikiweza tu kusema jambo sahihi, nitapata mkufu huo wa dhahabu"?

137 Loo, wewe, unaweza kuona mahali ilipo, leo? "Kama ningeweza kuyafurahisha masikio ya watu wangu, yaweke kando mambo haya. Sijali wanachofanya; wanalipa sana katika ha—hazina. Wanafanya *hivi, vile,* ama *vinginevyo*. Tutajenga kanisa kubwa mno, na kuweka mzunguko mkubwa juu yake. Tutafanya *hili, lile,* au *linginelo*."

138 Ee Mungu, uwarehemu watu kama hao. Nipe Ukweli. Naam. "Loo, tukizungumza jambo kama Hilo, ndugu, watu—watu wetu wangeamka na kutoka nje." Hawatatoka kama wanampenda Mungu. Watapenda kulisikia.

139 Mtu wa kweli wa Mungu haangalii *huku* na *huko*. Haangalii kuona kama mtu anasema, "Hiyo ni nzuri. Unaendelea vizuri." Au kuona kama mtu anasema, "Loo, hukupaswa kufanya hivyo." Hajali mtu yeyote anasema nini. Anafurahia ushirika wa Roho Mtakatifu, na anaangalia tu juu na kuendelea. Hajali kile mhubiri anasema, au kile ambacho watu wengine wanasema. Anafurahia ushirika wa Yule aliyemtuma. Hiyo ni kweli. Anapaswa kumpendeza Mmoja tu.

140 Tazama hii. Alisema, "Loo, Belteshaza, ulipaswa kujua vizuri zaidi kuliko haya. Je, hujui baba yako, Nebukadneza . . . " Ambaye, kwa kweli alikuwa babu yake. Akasema, "Je, hujui baba yako . . . " Ambayo, ilikuwa ni mfululizo wa wafalme. "Belteshaza, hujui vizuri zaidi? Ulikuwa na mfano huko nyuma, kwa yale Mungu aliyomtendea baba yako alipokuwa na kiburi, majivuno, na kuacha ufalme wake uende namna hiyo. Una mfano wa kile alichofanya."

141 Na kwa hivyo unao mfano wa kile Mungu alichofanya kwa wale ambao hawakutembea sawasawa mbele Zake. Haya si mambo ya siri. Huu sio Ujumbe mgumu. Ni Ukweli. Una mfano. Unajua alichofanya huko nyuma, kwa wanawake

waliocheza mbele ya sanamu. Unajua alichowafanyia wanaume waliowafuata wanawake wa ajabu. Unajua alichowafanyia walevi, na mashoga, na wapotovu wa Sodoma. Sio jambo la kigeni. Unajua mambo haya.

142 Akasema, "Ulipaswa kujua. Huo hapo mfano wako, kwa babu yako. Lakini, sasa, hii ndiyo maana ya maandishi hayo, 'Mungu amehesabu ufalme wako. Umepimwa katika mizani na umeonekana kuwa umepungukiwa.'"

143 Loo, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, Wapentekoste, wamepimwa katika mizani, mizani ya Mungu, na kuonekana wamepungukiwa! Wamemwita Roho wa Mungu aliye hai, "Kitu kichafu." Wamezichukia kazi za neema. Wamefuata makanisa makubwa na mashirika. Ninyi Assemblies of God, ninyi Church of God, ninyi nyote, ninyi wa umoja, na wa utatu, Wabaptisti, Mpresbiteri, Wakatoliki, mnajua mmerudi Babeli. Mlikuwa na mfano wa hilo.

144 Na Maskani hii ya Branham inajua ya kwamba mmeonywa juu ya mambo hayo, miaka mingi iliyopita, lakini sasa mmepimwa katika mizani na mmeonekana kuwa mmepungukiwa: kuzozana, kupigana, kushikilia vinyongo, na kuwa na hamaki. Mnafikiri Mungu angeweza kufanya kazi mahali kama hapo? Hasha. Haya basi.

145 "Wasiojali, wasio watakatifu, wasio na upendo wa asili, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji." Hiyo ndiyo siku tunayoishi.

146 Lakini kumbukeni, alisema, "Unajua hili." Lakini wakati huo huo, Danieli alikuwa akitoa unabii wake na kumwambia mfalme huyo. Je, unaweza kumwazia akiipaka sukari kote, kupata mkufu wa dhahabu? Je, unaweza kuwazia mtu wa Mungu akipatana na ibilisi, ili kuwa maarufu? Hasha.

147 Mnaweza kuwa na televisheni zenu, vipindi vyenu. Mnaweza kuwa na makanisa yenu makubwa. Mnaweza kuwa na chochote mtakacho. Hebu nisiwe maarufu, Mungu, bali hebu niwe mwaminifu kwa Roho Mtakatifu, kusema Kweli. Sijali kinachofanyika wala kiendacho. Tuna jambo moja la kufanya, hilo ni kutekeleza agizo la Bwana wetu mbarikiwa.

148 Lakini sisi hapa. Tuko katika siku hii, na ni juu yetu. Hakuna kinachoweza kufanywa sasa. Tumekwisha kuvuka mstari. Ni hali ya jinsi gani! Taifa linalundikana katika dhambi na upumbavu. Maandiko ya mkono yako ukutani. Roho wa Mungu akijifunua Mwenyewe, na watu wakirudi na kusema, "Ni Beelzebuli."

149 Yesu alisema, "Alinena. . .ukisema hayo dhidi Yangu, nitakusamehe. Lakini Roho Mtakatifu atakapokuja, hata neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao." Mfano mzuri wa hilo kwenye Pentekoste,

baada ya Pentekoste; na kisha wakati Tito, mwaka wa 96, alipoziteka kuta za Yerusalemu; walipokataa ujumbe. Hakika.

150 Sisi hapa. Na wakati ule ule unabii ulipokuwa ukitolewa. Sikiliza sasa, katika kufunga. Unabii ulipokuwa ukitolewa, ni nini kilifanyika? Nini kilifanyika? Wakati ule ule unabii huo ulipokuwa ukitolewa, Wamedi na Waajemi walikuwa wakija chini ya lango. Walinzi wa hekalu walikuwa wamechinjwa. Walinzi wa ngome waliuawa, mitaani.

151 Sikiliza. Dakika kumi baadaye, wale wasichana wa kisasa, warembo, wale wanawake wa kisasa mbali na watoto wao wachanga na watoto, nini kilitokea? Ni nini kilikuwa kikifanyika? Wangebanwa mitaani. Walibakwa na askari. Matumbo yao yalipasuliwa. Na fedheha iliyoletwa juu yao, kwa sababu hawakusikia. Lakini ilikuwa mbali sana.

152 Sikiliza, rafiki. Hakuna kitu saa hii hii, katika dakika ishirini na tano zijazo, ama dakika kumi, kwa Urusi kutuma satelaiti yake na kufagia hapa katika taifa hili, kuelekeza kombora lake, sema, "Jisalimishe, au baada ya dakika mbili hutakuwa chochote ila vumbi." Wanaweza kuifanya sasa hivi. Wazia hilo. Wanaweza kuifanya sasa hivi. Nini kingetokea? Mzigo wa ndege baada ya mzigo wa ndege, mzigo wa meli baada ya mzigo wa meli, wa askari wasiomcha Mungu wa kikomunisti, wangejaza nchi yetu, wangenyakua wasichana wetu na kuwapeleka barabarani, na kuwatendea kama ng'ombe, kuwachoma upanga. Waingie ndani ya nyumba zetu na kuwatoa wake zetu nje, na kukipiga kichwa cha mtoto mchanga ukutani, wawabake wanawake wetu. Unasema jambo moja? Ni mali yao.

153 Unasema, "Pentagon yetu itajisalimisha?" Hakika, ingejisalimisha. Hilo lingekuwa ndilo jambo pekee la busara kwake kufanya. Ingebidi kufanya hivyo. Ikiwa haikuwa hivyo, tungekuwa si kitu ila unga kwa dakika chache. Labda tungekuwa na saa chache zaidi za maisha, lakini ni mauaji yaliyoje!

154 Nini? Huenda wanapakia kwenye ndege sasa hivi. Meli zinaweza kuwa bandarini. Hivi karibuni mambo haya ambayo tunazungumzia yanaweza kuwa uhalisia. Hakuna jambo hata moja lililosalia, ili litendeke, kulifanya lisitokee kulingana na unabii. Sisi hapa. Na wiki ijayo hujui unaweza kuwa katika hali gani. Maandiko ya mkono yako ukutani. Tumepimwa katika mizani na kupatikana tumepungukiwa.

155 Sasa, kama mambo haya ni kweli, na unaona ni kweli, basi Kuja kwa Bwana kumekaribia kiasi gani? Usiku wa leo, nataka kuendelea. Nini? Je, Kanisa litakuwa wapi wakati haya yakifanyika? Sasa, ninyi ambao daima mmefikiria ya kwamba Kanisa litapitia Dhiki kuu, njoni mjue. Ikiwa hii ni karibu sana, ikiwa uharibifu huu umekaribia sana, ni kwa kiasi gani Kuja kwa Bwana kumekaribia zaidi? Kwa maana itatendeka kabla ya

Kanisa kuwahi . . . Kabla ya roketi moja kuipiga nchi hii, Kanisa litakuwa katika mikono ya Kristo, na kuondoka. Tuko mwisho. Inaweza kutokea wakati wowote.

Na tuombe.

156 Nataka watu wenye mawazo ya kilindi hapa ndani. Nataka wale walio . . . ujue kabisa kwamba Mtu huyo amekuwa akiongea nawe katika dakika chache zilizopita. Akisema, “Ndiyo, nimekuwa makosani. Nami ninataka kuwa sawa, na Mtu huyo, kwa maana Yeye Ndiye pekee ambaye anaweza kusoma mwandiko huu. Nataka kuwa sawa.” Je, unaweza tu kuinua mkono wako? Useme, “Niombee, Ndugu Branham.”

157 Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, kijana. Mungu akubariki, mama; wewe, wewe. Hiyo ni sawa. Mungu akubariki. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki, ewe kijana huko nyuma, msichana tineja. Mvulana mdogo, Mungu akubariki. Uko tu kwenye mabadiliko ya maisha.

158 Loo, inaweza kutokea, na itatukia. Haina budi kutokea. Na nyuzi hizi nyepesi ambazo unatembea juu yake zitakatika, mpenzi. Na maskini roho yako isiyojiweza, nini kitakufanyikia? Wakati hautakuwako tena. Wakati utaungana katika Umilele basi. Maandiko ya mkono ukutani; thibitisho la kisayansi. Wanajaribu kufika kwenye mwezi, kama walivyofanya huko Babeli. Kila kitu kinajirudia. Mungu wa Mbinguni hawezi kunyamaza tena. Wakati umewadia. Lini? Sijui; lakini wakati umewadia.

> Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa Mungu wanaukana,
> Ya kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu wetu;
> Siku hizo za Wamataifa zimehesabika, zimekumbwa na hofu;
> “Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”
>
> Siku ya ukombozi imekaribia,
> Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
> Mjazwe na Roho, taa zenu zikiwa zimesafishwa na kuwa safi,
> Tazameni juu, ukombozi wenu umekaribia.

159 Muda umeenda kuliko unavyofikiria. Je, si sasa hivi, chini ya sadikisho, kama unahisi kwamba umekuwa makosani; sijali ni muda gani umekuwa mfuasi wa maskani hii, sijali ni muda gani umekuwa mfuasi wa kanisa lako, ni mara ngapi umenena kwa lugha, ni mara ngapi ulicheza katika Roho; kama bado ungeweza kuona ulimwengu ukining’inia juu yako, njoo hapa kwa dakika moja tu. Njoo hapa, kondoo uliyepotea. “Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.” Je, ungeweza kuja hapa kwa

dakika moja, uniruhusu nikupe mkono? Simama hapa, na hebu tuombe pamoja. Ninakualika. Ondoka kwenye kiti chako moja kwa moja sasa na uje hapa; kama unapendezwa na maombi yangu. Ninakualika uje.

160 Hiyo ni sawa. Bwana akubariki, ndugu yangu mpendwa. Simama papa hapa madhabahuni kwa muda kidogo. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Ubarikiwe. Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu awabariki, nyote wawili. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Simama papa hapa madhabahuni sasa. Mungu akubariki.

161 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...akaikamata hapo hapo. Kama hatufahamiani mmoja na mwenzake, inua mkono wako. Hiyo ndiyo shida yako, sivyo? Sawa. Una imani. Unatoka kule Kentucky. Mungu akubariki. Roho Mtakatifu!

162 Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama.

Siku ya ukombozi . . .

163 Mungu akubariki, mama. Mungu awabariki, nyote wawili. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . kusoma akili"?

164 Kama huyo si Roho wa Kristo, sijui Yuko wapi. Kwa nini unakawia na kungoja basi? Hivi huwezi kuona ni Yeye? "Mambo nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya." Na hii ilikuwa ndiyo ishara ya wakati wa mwisho. Lisikilize, usiku wa leo, na uone kama hii si ishara ya wakati wa mwisho.

165 Njoo, sivyo? Ninyi mnaoamini ya kwamba Mungu amesema na moyo wenu, asubuhi ya leo, akisema, "Unapaswa kuona aibu kufanya mambo ambayo umefanya," utatoka nje?

"Vema," unasema, "Ningechukia da—dada yangu kuniona."

166 Vipi kuhusu Bwana wako? Loo, unataka kuokolewa, hutaki kwenda kuzimu ya shetani, lakini hutampokea kama Bwana wako. *Bwana* ni "mtawala." Bwana huchukua mamlaka yote. Unataka kuwa na maskini maisha yako ya kibinafsi. Unataka kuishi maisha ya Kikristo jinsi unavyotaka, lakini hutaishi jinsi Yeye anavyotaka uishi. Mwache aingie moyoni mwako. Na kusema, "Loo, ni—nimekukaribisha ndani ya moyo wangu, Yesu, kama Mwokozi wangu, ndiyo; lakini sijakuacha kamwe uwe na mamlaka, maana nilitaka kutenda kidogo *hivi*. Nataka kuwa wa kisasa." Loo, Yeye si Bwana wako, bado. Roho ya Elvis Presley na Godfrey bado imekushika; ibilisi. Hakika. Je, hutakuja ambapo Kristo anasonga? Mwone Roho Wake.

Roho Mtamu, fagia juu ya nafsi yangu.

Juu ya nafsi yangu . . .

167 Je, hutaomba? Najua unafikiri mimi ni . . . nina shida. Lakini, ninapoweza kuona kanisa, na kanisa lisilojali! Unadhani nini kingefanyika kama—kama George Washington, katika siku zake, angeona jambo lile lile likitukia ambalo ndiyo kwanza litukie papa hapa? Unafikiri watu wenye haki, na watu wakuu wa miaka iliyopita, wangefanya nini? Charles G. Finney alipopaza sauti neno moja, "Tubu au uangamie," na watu wakazimia mtaani.

168 Na, leo, Roho Mtakatifu anaweza kuweka maandishi ukutani, na kujionyesha Mwenyewe kuwa yuko, na wanaume huketi pale na kutazama huku na huku, enyi wanawake? Loo, ni baridi. Lakini kumbukeni, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, walikuwako wanane waliookolewa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

169 Mwaliko wako ni, "Njoo." Ninakualika madhabahuni pamoja na hawa wengine. Ikiwa unajua kwamba umekosea, kwa nini usije? Simama hapa, onyesha Mungu uko tayari kufanya juhudi. Lakini kama Roho Mtakatifu hawezi, basi najua siwezi.

Kwa hiyo na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

170 Nataka kumwombea mwanamke huyu. Ameinua mkono wake, hapa kwenye kitanda.

171 Dada yangu, Yesu Kristo anaweza kuokoa maisha yako, katika uzee huo, unaona. Je, unaamini ya kwamba atafanya hivyo? Nawe unajua hilo? Ikiwa mimi ni mtumishi Wake . . . Alisema katika Neno Lake, "Uambie mlima huu, 'Ng'oka,' wala usiwe na shaka, lakini uamini kwamba ulichosema kinatimia, kinaweza kuwa chako kile unachosema." Je, utamtumikia maisha yako yote? [Dada huyo anasema, "Nitamtumikia."—Mh.] Mpe Yeye pekee siku zako zilizosalia.

172 Bwana Mungu, ninapomshika mkono mwanamke huyu aliyelala hapa, anakufa, huenda hata asidumu hadi ibada ya usiku wa leo usipomsaidia. Namuona mnyonge sana hata hawezi kuketi; inabidi alale. Na kisha Wewe ulisema, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule. Mungu atawainua." Ninaomba ya kwamba utamponya mwanamke huyu sasa hivi. Na katika moyo wangu maskini, kama nilivyojua Roho Wako yuko hapa, ninauambia ugonjwa wa mwili wake, "Ondoka, katika Jina la Yesu Kristo, ili dada yetu aweze kuishi." Kuanzia saa hii, mateso na udhaifu viondoke. Jalia apone, kwa utukufu wa Mungu. Kupitia Jina la Yesu Kristo.

173 Neno limesemwa. Lengo langu na nia, nijuavyo mimi, ni sahihi. Basi, huyo hakuwa mimi; huyo alikuwa ni Yeye. Basi, ningeendelea na shughuli yangu, nikishangilia. Sahau yote kuhusu kuwa mgonjwa. Inuka, chukua kitanda chako, nenda nyumbani, ukishangilia. Ngoja kwa ajili ya ibada, usiku wa leo, mwangalie Bwana Mungu.

174 Ee Mungu, ukisimama katikati ya saa hii ya mauti, mauti kwa dhambi, mauti kwa kutokujali, mauti kwa magonjwa, kuondoka kwa magonjwa; Roho wako mkuu hapa, akifasiri hali zao! Ninawaombea hawa wanaosimama madhabahuni, wanaojua kwamba maandiko ya mkono kwenye ukuta ni hakika. Haiwabidi kuchukua neno langu kwa ajili yake. Wanalo Neno Lako sasa. Wanalo neno la gazeti. Wanalo neno la wanasayansi. Nasi tunajua, Kwako, uwe Mungu wa haki, huwezi kuiacha Babeli katika hali yao bila kuwapa hukumu yao, na wala hutatuacha tuende bila sisi kupata hukumu yetu.

175 Nasi tunaomba asubuhi ya leo, Baba, ya kwamba hawa waliosimama hapa wataepuka hukumu hiyo, wanapokuja salama chini ya mikono ya Yesu. Wanapokuja kumsikiliza Mtu anayeweza kufasiri mambo ya kiroho, ya kimbinguni. Wameisikia Sauti Yako ikinena, na wamekuja kukusikiliza Wewe. Uliponena, waliinuka kutoka kitini mwao. Wanakuja. Hawana aibu. Baadhi yao, Bwana, wamekuwa Wakristo kwa muda mrefu, lakini wao—hawaoni aibu kushuhudia kwamba wamekosea. Nawe umesema, "Mkinishuhudia mbele ya watu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba na Malaika watakatifu." Uwe na rehema, Ee Mungu wa Milele, na uwape Uzima wa Milele hawa wanaoutafuta sasa. Mioyo yao ya thamani na ijazwe na wema wa Mungu. Ninawawasilisha Kwako, Bwana.

176 Wamefanya jambo sasa hivi ambalo limekiuka kanuni zote za sayansi. Waliinuka kutoka kwenye kiti chao na kutembea hapa. Mikono yao iliinuliwa juu; inaonyesha kuna roho ndani yao, inayotembea. Na huyo roho anayewasukuma, ameshawishika, na Neno la Mungu, ya kwamba wamekosea. Matendo yao yamethibitisha kwamba wanatambua kuwa wamekosea. Nao walikuwa na kicho na heshima ya kutosha, wenye heshima, kuja madhabahuni, kuungama makosa yao na kuomba rehema. Wewe hutawakataa kamwe. Jalia, Bwana, kwamba kila mmoja ajazwe sasa na Roho Wako. Katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu.

Sasa wakati tumeinamisha vichwa vyetu.

177 Nashangaa, ninyi mnaosimama hapa, asubuhi ya leo, kwamba mnahisi ya kwamba mmefanya jambo lililo sahihi. Umekuja kwa mwaliko, si wa ndugu yako, bali umekuja kwa mwaliko wa Mungu mkuu, mtakatifu. Na kwa sababu umefanya hivi, na Roho Wake amekuita kutambua ya kwamba umekosea, nawe unataka kuwa sahihi. Na umemuomba Yeye aliyesema, "Mtu akipungukiwa na hekima, na aombe Mungu. Mwombeni Baba lolote, katika Jina Langu, nitalifanya." Ukija na huo moyo mnyofu, imani yako ikiegemezwa kabisa juu ya Neno la Mungu, unaamini kwamba sasa unapokea kile unachoomba? Mkipenda, huku mmeviinamisha vichwa vyenu, naomba mumwinulie Mungu mikono yenu, mseme, "Sasa

naamini." Mungu akubariki. Hilo ni sawa. "Sasa ninaamini kwamba nimepata kile nilichoomba."

178 Neema ya Mungu itajirishe nafsi zenu, ibariki roho zenu, na kuwafanya kuwa Wake Milele, katika Ufalme, katika ulimwengu ujao. Naomba ninii yenu. . . Neema yake ya Milele isiwaache kamwe. Na awadumishe katika saa za majaribu. Na kama bomu kubwa litapiga, na wakati mkuu utakuja, na utwaliwe katika kunyakuliwa kwa Kanisa Lake lililobarikiwa, kuwa pamoja Naye milele.

179 Ninyi katika wasikilizaji, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, na mngependa kukumbukwa katika maombi, ingawa hamkujitokeza lakini ungependa kukumbukwa, naomba mwinue mikono yenu. Hivi. . . Mungu akubariki. Unajua. . . Angalia tu mikono, asilimia tisini ya wasikilizaji.

180 Je, unatambua kuwa huu ni wakati wa kuchunguzwa? Huu ni wakati ambao hatuna budi kuchunguzwa. Huu unaweza kuwa ujumbe wa mwisho wa Injili unaohubiriwa. Kabla ujumbe haujaanza usiku wa leo, mwajua, bomu hilo linaweza kuipiga dunia. Hakuna kitu cha kuzuia kuwa hivyo. Yamewekwa. Yako tayari. Yote yanayohitajika ni vinywaji vichache vya Vodka, na hapa ingekuja. Na kitu pekee kinachoizuia, sasa hivi, ni neema ya Mungu kujaribu kuliunganisha Kanisa Lake. Hivi hutanisikia kama ndugu yako? Sikia Maandiko, kama Mwokozi wako, na umruhusu Kristo awe Mtawala mkuu katika maisha yako. Tujalie, tunapoomba.

181 Ombeni sasa, kila mmoja, kwa njia yako mwenyewe. Kama wewe ni Mbaptisti, omba jinsi Wabaptisti waombavyo. Haileti tofauti yoyote. Wewe omba tu. Unasema, "Mungu awe. . . " Sio wakati wa kubishania madhehebu sasa; tumekwisha kupita wakati huo. Sisi ni. . .

Njoo, ndugu.

182 Wakati tumesimama hapa. Sio sawa kwa mwinjilisti. . . Ambapo, bila shaka, baada ya kitambo kidogo, kutakuwa na ubatizo. Jumapili ya Pasaka ninakusudia kuwa hapa kwa ubatizo mkubwa. Na kama hujawahi kumpokea Kristo na kuzamishwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na unatamani kubatizwa kwa kuzamishwa, tunakualika uje. Hata sasa hivi, ikiwa unataka, tuko tayari.

183 Mchungaji lazima awe na kitu cha kusema. Nitamwomba aombe maombi haya, tunapongojea. Vema, Ndugu Neville.

*Yale Maandiko Ya Mkono Kwenye Ukuta* SWA58-0309M
(The Handwriting On The Wall)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 9 Machi, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org